**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

*APRILI, 2017*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya, uzima na nafasi nyingine ya kukutana hapa Dodoma katika Mkutano huu wa Saba wa Bunge la 11.

**Mheshimiwa Spika**, Pili kwa niaba ya Kamati yangu ninaomba kutoa pole kwako binafsi na kwa Wabunge wote kwa kuondokewa na Mbunge mwenzetu Dkt. Elly Marko Macha, Mbunge wa Viti Maalumu (CHADEMA) aliyefariki tarehe 31 Machi, 2017 huko Uingereza. Kamati pia inatoa pole kwa ndugu wa marehemu kwa msiba huu mzito.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee naomba kutoa pongezi za dhati kwa Mjumbe wa Kamati hii, Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Mb, ambaye ameteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Tunamtakia Utumishi Uliotukuka katika dhamana hii aliyopewa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati naomba kutoa pongezi za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki ambao wamechaguliwa kwenda kuiwakilisha Tanzania katika Bunge hilo.Tunawatakia Utumishi mwema katika Bunge la Afrika Mashariki na tunatoa rai kwao wakasimamie maslahi ya Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Maslahi mapana ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 6 (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Katiba na Sheria

jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu.

Aidha, Kanuni ya 7(1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 inatoa Mamlaka kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia. Jukumu hili la Uchambuzi wa Bajeti linaendana sambamba na jukumu la ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha unaoisha kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, iliyotengewa na kupokea fedha katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 kuanzia tarehe 22 hadi 24 Machi 2017. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Bajeti za Wizara na Taasisi inazozisimamia kuanzia tarehe 29 Machi hadi 02 Aprili 2017 ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu ina Mafungu 6 ya bajeti kama ifuatavyo;

i) Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu
ii) Fungu 25 - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu
iii) Fungu 65 - Kazi na Ajira
iv) Fungu 15 - Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA)
v) Fungu 61 - Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC)
vi) Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo Manne yafuatayo:-

i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na;

iv) Maoni na Ushauri wa Kamati

## 2.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 98 (1) inazitaka Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha unaoisha. Katika kutekeleza masharti ya Kanuni hiyo, Kamati ya Katiba na Sheria ilitembelea, kukagua na kupokea taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo inayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu tarehe 22 na 23 Machi 2017. Miradi hiyo ni:-

i. Mradi Na. 4494 – Ujenzi wa Soko na Barabara Pemba (Fungu 37)
ii. Mradi Na. 4494 - Ujenzi wa Soko na Barabara Unguja (Fungu 37)
iii. Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (Fungu 65)

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na miradi iliyoko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kamati ilitembelea na kukagua Miradi mingine ya Maendeleo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Katiba na Sheria. Katika Taarifa hii Kamati inajikita kutoa matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kama ilivyotajwa hapo juu.

### 2.1 Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inatoa maelezo ya kina kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa, gharama za hiyo miradi na namna miradi hiyo inavyosaidia Wananchi wa sehemu husika kama ilivyoelezwa katika kila mradi.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ufinyu wa muda wa kukagua Miradi ya Maendeleo Kamati ililazimika kujigawa katika makundi mawili; kundi la kwanza lilikwenda Pemba na kundi la Pili lilikwenda Unguja.

## 2.2 Miradi ya Ujenzi wa Soko na Barabara (Pemba)

**Mheshimiwa Spika**, kundi lililokwenda Pemba lilikagua miradi ya Ujenzi wa Soko na Barabara zilizo chini ya Mradi wa Marketing Infrastructure, Value Addition and Rural Financing Support Programme (MIVARF) ambao ni mradi wa kuboresha Miundo Mbinu ya Masoko, Uongezaji Thamani Mazao na Huduma za Fedha Vijijini. Mradi huu unatekelezwa katika Wilaya zote za Unguja na Pemba na unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD).

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Pemba Mradi huu umegharamia Ukarabati wa Barabara 19 zenye urefu wa Km 80. Ukarabati wa Barabara hizi umegharimu kiasi cha Shilingi Bilioni 6.4 za Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ufinyu wa muda, Kamati iliweza kukagua sehemu tu ya barabara hii yenye urefu wa Km 4.8 kutoka Chanjamjawiri mpaka Matale ambayo imegharimu **Shilingi Milioni Mia Tatu Themanini na Nne, Laki Sita na Sabini na Mbili, Mia Mbili na Hamsini na Mbili (384,672,252.24/=).** Barabara hii inatoa huduma kwa wazalishaji wa Shehia za Matale, Pujini, Dodo, Chonga na nyinginezo. Kabla ya kukarabatiwa barabara hii magari makubwa na madogo hayakuweza kupita kutokana na ubovu uliokuwepo na badala yake usafiri wa Punda na Mikokoteni ulikua unatumika kusafirisha mazao na watu. Baada ya Ukarabati wa barabara hii magari makubwa na madogo yameanza kutumia barabara hii kwa ajili ya usafirishaji wa mazao na hivyo kuongeza wigo wa masoko na faida kwa wazalishaji wa maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilitembelea mradi wa Soko la Tibirinzi, Chake Chake Pemba ambalo limejengwa kwa fedha za MIVARF. Gharama ya ujenzi wa Soko hili ni **Shilingi Milioni Mia Tisa Sabini na Mbili (972,000,000/=).** Soko hili linahudumia Mkoa wote wa Kusini Pemba na ujenzi wa Soko hili unatarajiwa kukamilika ifikapo Julai, 2017. Soko hili kama mengine yanayojengwa litakuwa na huduma ya chumba cha baridi kwa ajili ya kuhifadhia na kuongeza thamani ya mazao ya mboga mboga, matunda na samaki. Aidha soko hili la Tibirinzi litakuwa na mtambo wa barafu ambao utatumika kuzalisha barafu ambayo itatumika kuhifadhia samaki kwa wavuvi na wachuuzi wa samaki.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilikagua ukarabati wa kituo cha ya uhifadhi na kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno (Post-Harvest Training Centre) kilichoko Pujini, Wilaya ya Chake Chake, Pemba ambacho kitatumika kutoa mafunzo ya mbinu bora za usindikaji na uhifadhi wa mazao mbalimbali ya kilimo yanayolimwa na Wakulima kwa ajili ya kupunguza upotevu na kuongeza thamani ya mazao yao kwa lengo la kuongeza kipato. Aidha Kituo hiki kitahudumia Wananchi wote wa Pemba ambao watakuwa wanapata mafunzo kwa awamu tofauti baada ya kukamilika kwake. Ukarabati wa Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Mazao wenye Thamani ya **Shilingi Milioni Mia Mbili Kumi na Nne (214,000,000/=)** unalipiwa kwa asilimia Mia Moja (100%) na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB).

## 2.3 Miradi ya Ujenzi wa Soko na Barabara Unguja

**Mheshimiwa Spika**, kundi la Pili la Kamati lilikwenda Unguja kukagua Miradi mbalimbali ya Maendeleo iliyojengwa kwa fedha za MIVARF. Miradi iliyokaguliwa kwa upande wa Unguja ni; Barabara ya Dongongwe mpaka Mchangani, Soko la Kinyasini, Unguja na barabara ya Chaani mpaka Donge.

**Mheshimiwa Spika**, barabara ya Dongongwe - Mchangani yenye urefu wa Kilometa 4 ni moja kati ya barabara zilizofanyiwa ukarabati ili kuwasaidia wazalishaji na wasafirishaji wa mazao mchanganyiko yakiwemo muhogo, ndizi na matunda kwa wazalishaji wa Shehia za Mchangani na Ghana. Kabla ya ukarabati wa kiwango cha kifusi Barabara hii ilikua ikitumika kusafirishia mazao kwa Mikokoteni na Baiskeli na wakati wa kiangazi tu. Mara baada ya ukarabati, barabara hii ilianza kutumiwa na idadi kubwa ya magari makubwa na madogo yanayobeba mizigo tofauti ikiwemo vifaa vya ujenzi (mawe/mchanga) pamoja na magari ya huduma za Watalii. Barabara hii ni moja kati ya Barabara zenye urefu wa Km 68 ambazo zimekarabatiwa Unguja kwa fedha za Mradi wa MIVARF kwa Thamani ya **Shilingi Bilioni Tatu na Milioni Mia Moja (3,100,000,000/=).**

**Mheshimiwa Spika**, Barabara ya Chaani-Donge yenye urefu wa Kilomita 6.7 ilipendekezwa kufanyiwa ukarabati mahsusi kwa ajili ya kuwasaidia wazalishaji

wa mananasi eneo la ekari 3,200 kuongeza Thamani katika mnyororo wake wa thamani (Value Chain). Jumla ya Shehia tano ambazo ni Dongwe Vijibweni, Donge Pwani, Chaani Kubwa, Chaani Masingini na Bandamaji zenye kaya 2,552 na Wakazi 12,968 zinafaidika na uwepo wa barabara kwa matumizi ya kilimo na shughuli nyingine za Kiuchumi na Kijamii. Aidha, maeneo inayopita barabara hii yanalimwa muhogo na mazao mengine.

**Mheshimiwa Spika**, Soko la Kinyasini linahudumia Mkoa wote wa Kaskazini Unguja pamoja na baadhi ya wakazi wa Wilaya ya Kati iliyo kwenye Mkoa wa Kusini Unguja. Aidha soko hili pia, linategemewa na Sekta ya Utalii kwa wamiliki wa mahoteli Ukanda wa Kaskazini Mashariki ya kisiwa hiki. Kwa mujibu wa Mkataba Mkandarasi anatakiwa kulikabidhi Soko hili pamoja na jengo la utawala ifikapo Julai 2017. Gharama ya ujenzi wa Soko hili ni **Shilingi Bilioni Mbili na Milioni Mia Tano (2,500,000,000/=)**.

### 2.4 Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ( WCF)

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 23 Machi 2017 Kamati ilitembelea Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi na kupokea Taarifa ya Utekelezaji ya Mfuko kwa Nusu ya Kwanza ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 (Julai -Desemba, 2016).

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) ni Taasisi ya Hifadhi ya Jamii iliyoundwa kwa mujibu wa Kifungu cha 5 cha Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi Sura ya 263 marejeo ya Mwaka 2015 ili kushughulikia masuala ya Fidia kwa Wafanyakazi waliopo katika Sekta ya Umma na Binafsi Tanzania Bara ambao wataumia, kuugua au kufariki kutokana na kazi wanazofanya kwa mujibu wa Mikataba ya Ajira zao.

## 2.5 Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, lengo la kufanya ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, pamoja na mambo mengine, ni kujiridhisha na uwepo wa miradi hiyo (Field inspection) na matumizi sawia ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge katika utekelezaji wa miradi hiyo. Kamati inapojiridhisha na uwepo wa miradi hii; na baada ya kulinganisha miradi hiyo na fedha iliyotumika katika kuitekeleza, inaweza kuishauri vema Serikali katika jukumu lake la kuleta na kusimamia maendeleo katika nchi.

## 2.6 Maoni na Mapendekezo ya Jumla Kuhusu Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** kwa Miradi ya Ujenzi wa Barabara na Masoko iliyoko Pemba na Unguja , Kamati kwa sehemu kubwa imeridhishwa na maendeleo ya miradi hii na inatoa rai kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Mradi wa MIVARF kukamilisha kwa haraka miradi hii ili Wananchi wengi wa maeneo husika waweze kufaidika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba Makandarasi wote waliopewa kazi ya ujenzi wa miradi hii ya Barabara na Masoko kwa upande wa Unguja na Pemba kukamilisha miradi hiyo ndani ya muda uliopangwa ili shughuli nyingine za Kiuchumi zinazotegemea kukamilika kwa miradi hiyo ziendelee na ziweze kuwasaidia Wananchi wengi katika uzalishaji na kuongeza kipato chao.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliona kwamba kuna haja kubwa ya kuhakikisha kwamba Thamani ya fedha iliyotumika katika miradi hiyo inaonekana. Katika mradi wa ujenzi wa Soko la Kinyasini Unguja Kamati ilitilia shaka aina ya Soko lililojengwa na kiwango cha fedha (**Bilioni Mbili Milioni MiaTisa)** kilichotajwa kutumika katika mradi huo. Kamati inatoa rai kwa Ofisi ya Waziri Mkuu

kujiridhisha na matumizi ya fedha hizo katika mradi huo na kufuatilia kama fedha iliyotengwa kwa ajili ya mradi huo ilitumika ipasavyo. (Value for money).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati kwa ujumla inawashukuru sana Wahisani wa mradi huu, Benki ya Maendeleo Afrika na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo kwa kutoa fedha za miradi hii. Kamati inatoa rai kwa Halmashauri na Mikoa yote inayohusika na utekelezaji wa miradi hii katika maeneo yao kutoa ushirikiano wa kutosha na kufuatilia kwa karibu usimamizi, utekelezaji na uendelevu (Sustainability) wa miradi hii katika kuwasaidia Wakulima na Wananchi wa maeneo husika.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupokea taarifa ya Utekelezaji ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, Kamati ilitoa maoni yafuatayo:-

- Mfuko uweke mkazo zaidi katika ulipaji wa Fidia kwa Wafanyakazi jambo ambalo ndio lengo kuu la Mfuko (Core Objective);

- Elimu kuhusu Mfuko iendelee kutolewa kwa Wananchi na Wadau wote ili Waajiri na Waajiriwa wengi wawe na ufahamu sahihi kuhusu Mfuko;

- Mfuko uchukue jitihada za kutosha kufanya kazi na Sekta Binafsi/isiyo rasmi ili kuongeza wigo wa watu wanaotumia huduma za Mfuko na kutii matakwa ya Sheria inayounda Mfuko;

- Mfuko uzingatie Sera au Miongozo ya Uwekezaji wa fedha za Mifuko (Investment Policies/Guidelines) ili kuwekeza kwa faida na kulinda uimara wa kifedha wa Mfuko (Financial Liquidity) na kulinda usalama wa fedha za Wanachama;

- Mfuko uchukue jitihada za kutosha kupambana na kudhibiti mianya yote ya rushwa hasa katika eneo la uwekezaji wa fedha za Mfuko na uendeshaji wa Mfuko kwa ujumla;

- Mfuko uhakikishe una ''Data Base - Kanzi Data'' sahihi ya idadi ya Waajiri Tanzania ili kuongeza wigo wa michango ya Fidia kwa Wafanyakazi;

- Mfuko uendelee kusimamia vizuri utekelezaji wa Sheria inayounda Mfuko pamoja na Kanuni zake.

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA OFISI YA WAZIRI MKUU KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa fedha 2017/2018, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 tarehe 29 na 30 Machi, 2017. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

### 3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ulitazama mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Aprili 2016 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi Machi 2017 katika Robo ya Tatu ya Mwaka huu wa fedha 2016/2017. Uchambuzi huu pia ulitazama kiasi cha fedha kilichoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 na kiasi cha Fedha kilichopokelewa katika Miradi ya Maendeleo hadi kufikia Mwezi Machi 2017. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa Mpango wa Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 ili kujua vipaumbele vya kibajeti katika mwaka wa fedha ujao.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati ulitazama pia eneo la ukusanyaji wa Maduhuli kwa kulinganisha kiasi kilichokusanywa hadi Machi 2017 na lengo la ukusanyaji lililowekwa wakati wa kupitisha bajeti Mwezi Aprili 2016. Lengo la uchambuzi wa namna hii ni kufahamu uwezo wa Serikali katika kukusanya Maduhuli. Kamati ilitumia njia mbalimbali katika uchambuzi wake kama kutazama hali halisi ya kila Taasisi, kujiridhisha na taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu kwenye Kamati.

### 3.2 Uchambuzi wa Taarifa Kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Bunge liliidhinisha Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli yenye jumla ya **Shilingi Bilioni Thelathini na Nane, Milioni Hamsini na Moja, Laki Saba na Tatu Elfu (38,051,703,000/=).** Hadi kufikia 28 Februari , 2017 kiasi cha Maduhuli kilichokusanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake ni **Shilingi Bilioni Ishirini , Milioni Mia sita Arobaini na Tatu, Laki Tisa Sabini na Nane MiaTano Sabini na Saba (20,643,978,577)** sawa na asilimia 54 ya lengo lililokusudiwa. Kamati imegundua kwamba ukusanyaji wa Maduhuli umepungua katika mwaka huu wa fedha ukilinganisha na Maduhuli yaliyokusanywa na Serikali mpaka kufikia Machi 2016 wakati wa utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2015/2016 ambapo lengo la ukusanyaji Maduhuli lilifikiwa kwa zaidi ya asilimia 100.

### 3.3 Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Mafungu yanayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zilizo chini yake

yalitengewa **Shilingi Bilioni Sitini na Nne, Milioni Mia Sita,Laki Tano Hamsini na Nne Elfu, Mia Tisa Arobaini na Nane (64,600,554,948 /=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Februari 2017 Taasisi hizo zilipokea **Shilingi Bilioni Thelathini na Saba,Milioni Mia Tano Thelathini na Sita, Laki Nne Elfu Tisa na Thelathini na Tisa (37,536,409,039)** sawa na asilimia 58 ya fedha iliyoidhinishwa.

**Uchambuzi wa uwiano wa bajeti iliyoidhinishwa na upatikanaji wa fedha ya Matumizi ya Kawaida hadi kufikia Februari 28, 2017 umeonyeshwa katika jedwali Na. 1**

**JEDWALI NA. 1**

| NA. | FUNGU | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | FEDHA ILIYOPATIKANA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 37-OFisi ya Waziri Mkuu | 23,857,728,000/= | 12,709,618,127/= | 53% |
| 2 | 25- Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu | 4,034,253,000/= | 2,966,702,626.2/= | 74.5% |
| 3 | 65 – Kazi, Ajira ,Vijana na Wenye Ulemavu | 11,561,196,000/= | 7,236,597,069/= | 63% |
| 4 | 27- Msajili wa Vyama vya Siasa | 19,624,351,948.2/= | 11,141,142,633/= | 57% |
| 5 | 15-Tume ya Usuluhishi na Uamuzi | 2,435,301,000/= | 1,415,295,800/= | 58.11% |
| 6 | 61- Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 3,117,626,000/= | 2,067,051,784/= | 66% |

Uchambuzi huu unaonyesha kuwa kumekuwa na upungufu wa upatikanaji wa fedha

kwa kila Fungu. Hali hii inaweza ikawa imesababishwa na Mipango isiyowiana na Matumizi halisi au ikawa imesababishwa na Serikali kuwa na makusanyo kidogo. Kamati inashauri Serikali kupanga bajeti kwa kuzingatia mapato ya Serikali na mahitaji halisi ya Taasisi husika.

### 3.4 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 37) ilitengewa jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Moja Hamsini na Tisa, Milioni Mia Moja Sabini na Nne, Elfu Kumi na Moja, Mia Sita Ishirini na Tisa (159,174,011,629/=)** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Februari 28, 2017 jumla ya **Shilingi Bilioni Sabini, Milioni Mia Nne Themanini na Nne, Laki Sita Thelathini na Nne Elfu na Thelathini na Sita (70,484,634,036/=)** sawa na asilimia 44 ya fedha iliyoidhinishwa ilipokelewa. Hali hii kwa kiasi kikubwa imechangiwa na kupungua kwa fedha za Miradi ya Maendeleo kutoka kwa Wahisani.

**Mheshimiwa Spika**, kuna miradi ambayo ilitengewa fedha za Maendeleo katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/2017, hadi kufikia Februari 28, 2017 baadhi ya miradi hiyo haikupokea fedha yoyote ya ndani wala ya nje. Miradi hiyo ni kama Mradi Na. 6510 kuhusu Uendelezaji wa Makao Makuu Dodoma (CDA), Mradi Na. 4945 Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na Mradi Na. 6577 Mradi wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

**Uchambuzi wa uwiano wa bajeti iliyoidhinishwa na upatikanaji wa fedha ya Maendeleo hadi Februari 2017 umeonyeshwa katika jedwali Na. 2**

**JEDWALI NA. 2**

| NA | MRADI | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | | FEDHA ILIYOPATIKANA | | Asilimia ya Fedha Iliyopokelewa | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | NDANI | NJE | NDANI | NJE | NDANI | NJE |
| 1. | Mradi NA. 4494.MIVARF | 50,000,000/= | 99,769,951,000/= | 0 | 38,462,065,529/= | 0 | 38.5% |
| 2. | NA. 6351 Ujenzi Ofisi ya Waziri Mkuu | 4,500,000,000/= | | 4,467,949,414/= | | 99.28% | |
| 3. | Na.5306 Mraddi wa kuimarisha taarifa na mabaddiliko ya tabia nchi na mifumo ya tahadhali | 0 | 1,929,852,000/= | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 4 | Na. 6575 mradi wa kujianndaa na kukabidhi maafa | 0 | 244,970,000/= | 0 | 153,300,000/= | | 62.5% |
| 5. | Na. 4937 kujenga uwezo wa mitambo ya uchapishaji | 150,000,000/= | | 29,644,000/= | | 19.76% | |

Uchambuzi huu unaonyesha kuwa fedha nyingi za Maendeleo zinategemea fedha ya nje hali ambayo inaleta utegemezi na ugumu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotegemea fedha za nje. Hali hii inasababisha miradi mingi kutotekelezeka kwa wakati. Ni mapendekezo ya Kamati kuwa Serikali ijitahidi kupunguza utegemezi kwa kutenga fedha yake ya ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha uchambuzi unaonyesha hata fedha ya ndani iliyoidhinshwa na Bunge haikuweza kutolewa kama ilivyokusudiwa kama inavyoonekana katika jedwali. Kwa mfano Mradi Na. 6510 kuhusu uendelezaji wa Makao Makuu Dodoma ulitengewa na kuidhinishiwa na Bunge kiasi cha Shilingi Milion Hamsini (50,000,000) hadi kufikia Februari 2017 hakuna fedha yoyote ilipokelewa. Hali hii inaweza ikawa imesababishwa na kupungua kwa mapato ya Serikali . Kamati inashauri kuwa ni vema Mipango ya Serikali ikaendana na utekelezaji.

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 tarehe 29 na 30 Machi 2017. Mpango huu wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 umeandaliwa kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 - 2020, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mpango ambao umelenga utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/2021).

### 4.1 Uchambuzi wa Vipaumbele vya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Bajeti wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 umeainisha maeneo 22 ya viapumbele yakiwemo;

i) Kujenga uwezo wa Serikali kukabiliana na Maafa;

ii) Kuratibu Utekelezaji wa Mpango wa Utoaji wa Shilingi Milioni Hamsini (50,000,000) kwa kila Kijiji/Shehia;
iii) Kuratibu Utekelezaji wa Mpango wa Ushiriki wa Watanzania kwenye Uwekezaji (Local Content);
iv) Kuratibu Shughuli za Bunge na kushughulikia kero na malalamiko ya Wananchi;
v) Kuratibu Utekelezaji wa Sera, Sheria na Mikakati ya Kukuza Ajira nchini na kuongeza nafasi za ajira za Watanzania nchi za nje
vi) Kuratibu na kusimamia Uwezeshaji na Maendeleo ya Vijana
vii) Kusimamia, Kuratibu na kutoa huduma kwa Watu wenye Ulemavu

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliridhishwa na Vipaumbele viliyowekwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu vinaendana na Mpango wa Taifa wa Mwaka 2017/2018 na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017-2020/2021). Kamati pia imeridhika na vipaumbele hivi kwa sababu vinajumuisha maeneo yote ya msingi ambayo yapo katika Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na vipaumbele hivyo Kamati inatoa rai kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba vipaumbele vyake vinaakisi Kauli Mbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuwa na Tanzania yenye Viwanda ili kuweza kutengeneza Ajira kwa Wananchi wengi na kuongeza fursa mbalimbali za biashara na mapato kwa nchi na Wananchi.

## 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Ofisi ya Waziri Mkuu inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi Bilioni Thelathini na Saba, Milioni**

**Mia Tano Hamsini na Nne, Mia Tisa Tisini na Nane na Mia Moja (37,554,998,100/=).** Maduhuli haya yatakusanywa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 37), Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Fungu 61) na Fungu 65 (Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu). Sehemu kubwa ya Makadirio ya Maduhuli haya yatatokana na shughuli za Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali katika kuchapa Nyaraka mbalimbali za Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, pamoja na Nyaraka za matukio maalumu. Sehemu nyingine inayotegemewa kutoa Maduhuli zaidi ni Fungu 65 ambalo linahusisha Taasisi mbalimbali zilizo katika Sekta ya Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu.

**Mheshimiwa Spika**, kiasi cha Maduhuli kinachotegemewa kukusanywa kutoka Fungu 65 ni **Shilingi Bilioni Thelathini na Tano, Milioni Ishirini na Tisa, Laki Sita Elfu Tano na Mia Moja. (35,029,605,100).**
Kiasi hicho ni pungufu ya lengo la Mwaka 2016/2017 kwa kiasi cha **Shilingi Bilioni Tatu,Milioni Ishirini na Moja,Laki Sita Ishirini na Nane Elfu na Mia Tatu (3,021,628,300 /=)** ambayo ni sawa na asilimia 8.6%

## 4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Ofisi ya Waziri Mkuu inaomba jumla ya **Shilingi Bilioni Sabini na Nane,Milioni Hamsini na Saba,Laki Saba Ishirini na Saba na Elfu,Mia Tatu Sabini na Saba (78,057.727,377/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Kumi na Sita, Milioni Mia Tano na Mbili, Laki Nne na Sabini na Sita Elfu, Mia Tatu Thelathini na Nne (16,502,476,334/=)** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi Bilioni Ishirini na Tisa, Milioni Mia Sita Kumi na Nane, Laki Nane Tisini na Tisa Elfu, Mia Tisa Kumi na Sita (29,618,899,916/=)** ni ruzuku kwa Taasisi zilizo chini

ya Ofisi ya Waziri Mkuu na **Shilingi Bilioni Thelathini na Moja, Milioni Mia Tisa Thelathini na Sita, Laki Tatu Hamsini na Moja Elfu, Mia Moja Ishirini na Saba (31,936,351,127/=**) ni fedha za Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** katika mchanganuo wa Mapato na Matumizi kwa Mafungu yaliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Mafungu ambayo yametengewa fedha nyingi kuliko mengine katika Mwaka wa Fedha ujao ni Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa (Fungu 27) ambalo limetengewa **Shilingi Bilioni Kumi na Tisa, Milioni Mia Nne Themanini na Mbili,Laki Tatu Kumi na Saba Elfu,Mia Saba Arobaini (19,482,317,740/=)** na Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 37) ambalo limetengewa **Shilingi Bilioni Ishirini na Moja, Milioni Mia Nane Tisini na Moja, Laki Nne Themanini na Tatu Elfu, Mia Saba Sitini na Nne (21,891,483,764/=).**

### 4.4 Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake zimeombewa **Shilingi Bilioni Themanini na Tatu, Milioni Mia Tano Sitini na Tano, Laki Tatu Sabini na Mbili Elfu,Mia Saba Sitini na Tatu (83,565,372,763/=)** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizi **Shilingi Bilioni Ishirini na Mbili, (22,000,000,000/=)** ni fedha za ndani na **Shilingi Bilioni Sitini na Moja, Milioni Mia Tano Sitini na Tano, Laki Tatu Sabini na Mbili Elfu, Mia Saba Sitini na Tatu (61,565,372,763/=)** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** fedha iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 ni pungufu kwa kiasi cha **Shilingi Bilioni Hamsini na Sita, Milioni Mia Tisa na Mbili, Laki Mbili na Arobaini na Saba Elfu, Mia Mbili Thelathini na Saba (56,902,247,237/=)** ya fedha iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambazo zilitengewa kiasi **Shilingi Bilioni Mia Moja Arobaini, Milioni**

**Mia Nne na Sitini na Saba, Laki Sita na Ishirini Elfu (140,467,620,000/=).** Kiasi hiki ni Pungufu ya Asilimia 40 ikilinganishwa na Bajeti ya Maendeleo kwa Ofisi ya Waziri Mkuu iliyoidhinishwa na Bunge hili Tukufu Mwezi Aprili 2016.

**Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Ofisi ya Waziri Mkuu katika Miradi ya Maendeleo katika Mwaka huu wa Fedha umelenga katika maeneo 8 yakiwemo:-

i) Kuboresha mandhari na Ujenzi wa Miundombinu ya Makao Makuu Dodoma;

ii) Kujenga uwezo wa Serikali kukabiliana na Maafa

v) Kuimarisha Ushindani katika Sekta Binafsi

vii) Kuendelea kuwajengea uwezo wa Kiuchumi Vijana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Ofisi ya Waziri Mkuu katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, miradi iliyopewa kipaumbele ni kama ifuatavyo; Mradi Na.6351 kuhusu Ujenzi wa Makazi ya Waziri Mkuu, Mlimwa - Dodoma uliotengewa **Shilingi Bilioni Tatu (3,000,000,000/=)** fedha za ndani, Mradi Na. 6581 kuhusu Programu ya Kukuza Ujuzi nchini uliotengewa **Shilingi Bilioni Kumi na Tano (15,000,000/=)** Fedha za ndani, Mradi Na. 4944 wa kuimarisha ushindani katika Sekta Binafsi uliotengewa **Shilingi Bilioni Kumi na Sita, Milioni Mia Mbili Hamsini na Nane Elfu, Laki Tano Tisini na Nne Elfu, Mia Nane Arobaini na Nne. (16,258,594,844/=)** fedha za Nje na Mradi Na. 4494 kuhusu Uendelezaji wa Mifumo ya Masoko na Huduma ya Kifedha Vijijini (MIVARF) uliotengewa **Shilingi Bilioni Arobaini na Mbili, Milioni Mia Nne na Arobaini na Tano, Laki Moja Hamsini na Tisa Elfu, Mia Tisa Kumi na Tisa (42,445,159,919/=)** ambazo ni fedha za nje kutoka Benki ya Maendeleo Afrika (ADB) na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD)

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo wa fedha za Bajeti ya Maendeleo kwa miaka michache iliyopita inaonyesha kwamba nchi imekua inategemea fedha za nje kuliko fedha za ndani. Katika Mwaka ujao wa fedha, Bajeti ya jumla ya Serikali kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni asilimia 38 ya Bajeti yote ambayo ni pungufu ya asilimia 2 ya bajeti ya maendeleo ya Serikali iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017. Kupungua kwa Bajeti ya Maendeleo ya Ofisi ya Waziri Mkuu kunachangiwa pamoja na sababu nyingine, na kupungua kwa utayari wa Wahisani na Wadau mbalimbali wa Maendeleo kutoa fedha za Miradi ya Maendeleo kutokana na mabadiliko mbalimbali ya Sera za nchi Wahisani na Taasisi za maendeleo za Kimataifa.

**Jedwali Na. 03: Ulinganisho wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na 2017/2018**

| **2016/2017** | | **2017/2018** | |
|---|---|---|---|
| Kawaida | Maendeleo | Kawaida | Maendeleo |
| 61,912,319,016/= | 140,467,620,000/= | 78,057,727,377/= | 83,565,372,763/= |

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi huu unaonyesha kuwa bajeti ya Matumizi ya Kawaida (Recurrent) imeongezeka kwa asilimia 19.3 % na bajeti ya Maendeleo imepungua kwa asilimia 40% ya malengo katika Mwaka uliopita wa fedha. Hali hii haiakisi Kauli Mbiu ya Serikali ya Uchumi wa Viwanda. Kamati inashauri Serikali kupanua wigo wa vyanzo vya mapato ili kuweza kufikia azma yake ya uchumi wa viwanda. Haiwezekani Serikali kujenga Uchumi wa Viwanda kwa kutegemea fedha ya Wahisani.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** ninaomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na Taarifa za Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake. Maoni na Ushauri wa Kamati pia umezingatia ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2016/2017.

## 5.1 FUNGU 37-Ofisi ya Waziri Mkuu

i) **Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa na Kamati kwa Ofisi ya Waziri Mkuu katika Mwaka wa Fedha uliopita. Aidha Kamati inatoa wito kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kufanya rejea ya maagizo ambayo hayakutekelezwa kikamilifu kuyakamilisha kwa wakati hususani upatikanaji wa Sheria ya Uanzishwaji wa Makao Makuu Dodoma, Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, Masuala yote ya Kukabiliana na Maafa na Maboresho mbalimbali ya Sheria.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kwamba Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ni Ofisi Muhimu katika kuendesha shughuli za Serikali lakini haijatengewa fedha ya Maendeleo katika Mwaka ujao wa Fedha. Kamati inaishauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba Ofisi hii inapewa kipaumbele katika Mpango wa Maendeleo wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kadri Upatikanaji wa Fedha unavyoruhusu.

iii) **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Umuhimu wa Ofisi na Shughuli za Waziri Mkuu, Kamati inashauri Ofisi ya Waziri Mkuu kukamilisha hatua iliyobaki ya ujenzi wa Makazi na Ofisi ya Waziri Mkuu hapa Dodoma katika Mwaka huu wa fedha (2017/2018)

iv) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kwamba mara tu miradi ya MIVARF inapokamilika katika maeneo husika,Watendaji wa Maeneo hayo waendelee kuisimamia miradi hiyo kwa ukaribu ili iweze kudumu na kuleta faida kwa Wananchi wengi zaidi.

v) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Zabuni za ujenzi wa Miradi ya Maendeleo zitolewe kwa uwazi (Transparent and Competitive Bidding Process) na kipaumbele kitolewe kwa Makampuni ya Ndani ya wakandarasi yaliyokidhi vigezo na yenye uwezo wa kutekeleza na kukamilisha miradi kwa wakati na kwa mujibu wa Mikataba ya Miradi husika.

vi) **Mheshimiwa spika**, katika Miradi yote ya Maendeleo iliyotengewa fedha Mwaka uliopita wa Bajeti (2016/2017) na ile iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha ujao (2017/2018), hususani Miradi ya MIVARF, Kamati inashauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba fedha zote za Miradi ya Maendeleo zinatumika kwa tija na kwa kuzingatia Kanuni ya thamani ya fedha kwa miradi husika (Value For Money).

## 5.2 Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa

i. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia mgogoro unaoendelea katika Chama cha CUF Kamati inashauri Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuchukua jitihada za kutosha kusuluhisha mgogoro huo ili kuepusha athari kubwa zinazoweza kujitokeza katika Muungano.

ii. **Mheshimiwa Spika**, Kamati pia inaigiza Ofisi ya Msajili wa vyama vya Siasa kuzingatia Sheria, Kanuni,Taratibu na weledi katika usimamizi na utoaji wa ruzuku kwa vyama vya siasa na kuhakikisha kwamba taratibu hizo zinafuatwa katika utoaji ruzuku kwa vyama vya siasa.

## 5.3 Mfuko wa Fidia Kwa Wafanyakazi (WCF)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Mfuko kuweka mkazo zaidi katika ulipaji fidia kwa Wafanyakazi ambalo ndilo lengo kuu la Mfuko na kuweka Mfumo mzuri wa kufanya tathmini za fidia kwa Wafanyakazi wanaopata ajali kazini na kuhakikisha kwamba malipo ya fidia yanafanyika kwa haraka kwa kila Mfanyakazi aliyetimiza vigezo vya fidia.

## 5.4 Fungu 65 - Kazi na Ajira

i) **Mheshimiwa spika**, kuhusu mpango wa kuunganisha Mifuko ya Pensheni, Kamati inaishauri Serikali kujiridhisha na masuala yote ya kitaalamu pamoja na kufanya mapitio na maboresho ya Sheria yanayohitajika katika kutekeleza mpango huu wenye nia nzuri ya kuwa na Sekta ya Pensheni imara na yenye ufanisi kwa Wafanyakazi wote. Kamati inatambua kwamba baadhi ya Mifuko ya Pensheni ina hali nzuri Kifedha (Financial Liquidity) na mingine ina hali mbaya Kifedha na madeni mengi (Liabilities). Sababu za Kitaalamu zizingatiwe ili mwisho wa siku maamuzi sahihi na ya kitaalamu yafanyike kwa faida ya mifuko yote na Wafanyakazi wote.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Mamlaka ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA) kuendelea kusimamia Afya na Usalama wa Wafanyakazi Mahali Pa Kazi na hasa kwa Wafanyakazi wanaofanya kazi katika maeneo hatarishi kama Migodini au Viwandani na kuchukua hatua kali za kisheria kwa Waajiri wote wasiozingatia masuala ya Afya na Usalama wa Wafanyakazi wao.

## 5.5 Fungu 61-Tume ya Taifa ya Uchaguzi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuendelea kuboresha Daftari la Wapiga Kura na kuchukua jitihada za kutosha katika uboreshaji wa Daftari hili. Hatua hizi zijumuishe utoaji Elimu ya Uraia hususan uandikishaji wa Wapiga Kura kwa Vijana wengi zaidi ili waweze kutumia haki yao ya Kikatiba ya kupiga au kupigiwa kura. Hali hii itaongeza idadi ya Watanzania wengi zaidi watakaokua na sifa na vigezo vya kupiga kura katika chaguzi mbalimbali zinazokuja.

# 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukupongeza kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili vema na kwa weledi wa hali ya juu. Nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Napenda nikupongeze pia kwa umahiri wako katika kasi ya

kuliendesha Bunge hili katika kutekeleza Kauli Mbiu ya **HAPA KAZI TU** na kuishauri vema Serikali kwa manufaa ya Wananchi wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Naibu Spika Mheshmiwa Tulia Ackson ,Mb, kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge. Niwapongeze pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge. Wote kwa pamoja tunawaombea afya na uzima katika kutekeleza majukumu mliyopewa.

**Mheshimiwa Spika**, nichukue fursa ya kipekee kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, na nimtakie kazi njema ya kuliongoza Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**, nimpongeze Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Majaliwa Kassimu Majaliwa kwa kazi nzuri anayoifanya katika kusimamia utekelezaji wa bajeti na shughuli za Serikali Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge Kazi, Ajira, Vijana, na Walemavu, Mhe. Jenista J. Mhagama, (Mb) Naibu waziri, Mhe. Antony Mavunde, (Mb), Makatibu Wakuu Ndg. Erick Shitindi (Kazi na Ajira) na Ndg. Hamisi H. Mwinyimkuu (Sera, Bunge na Uratibu) pamoja na Wataalam wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Napenda pia kumtakia utumishi mwema Ndg. Maimuna Tarishi ambaye ameteuliwa na Mhe. Rais kuwa Katibu Mkuu,Ofisi ya Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na

Walemavu. Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie Katika Hansard:-

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb – M**akamu /Mwenyekiti**
3. Mhe. Ajali Rashid Akbar, Mb - Mjumbe;
4. Mhe. Ally Saleh Ally, Mb - Mjumbe;
5. Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb - Mjumbe;
6. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe;
7. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb - Mjumbe;
8. Mhe. Juma Hamad Kombo, Mb - Mjumbe;
9. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb - Mjumbe;
10. Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb - Mjumbe;
11. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb - Mjumbe;
12. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe;-
13. Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb - Mjumbe;
14. Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb - Mjumbe;
15. Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb - Mjumbe;
16. Mhe. Wanou Hafidhi Ameir, Mb - Mjumbe;
17. Mhe. Riziki Shahari Mngwali, Mb - Mjumbe;
18. Mhe. Saumu Heri Sakala, Mb - Mjumbe;
19. Mhe. Seif Ungando Ally, Mb - Mjumbe;
20. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb - Mjumbe;
21. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb - Mjumbe;
22. Mhe. Twahir Awesu Mohammed, Mb - Mjumbe;
23. Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb - Mjumbe
24. Mhe. David Mathayo David, Mb - Mjumbe
25. Mhe. Ussi Pondeza,Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, mwisho, kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Angelina L. Sanga, Makatibu wa Kamati hii, Ndg. Stella Bwimbo, Ndg. Dunford Mpelumbe na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii. Napenda pia kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) Ndg. Hanifa Masaninga na Watendaji wote wa Idara hiyo kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inatoka wa wakati na kwa ubora.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera,Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb.

**MWENYEKITI,**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**

06 APRILI, 2017